




(uten bilder)

✎ Ghanaian folktales
🔒 Wiehan de Jager
📄 Mutugi Kamundi
🗣️ swahili
📖 nivå 3



Anansi na hekima



Barnebøker for Norge


barnebøker.no

Anansi na hekima


Skrevet av: Ghanaian folktales
Illustrert av: Wiehan de Jager
Oversatt av: Mutugi Kamundi

Denne fortellingen kommer fra African Storybook (africanstorybook.org) og er videreformidlet av Barnebøker for Norge (barnebøker.no), som tilbyr barnebøker på mange språk som snakkes i Norge.


Dette verket er lisensiert under en Creative Commons Navngivelse 3.0 Internasjonal Lisens.
<https://creativecommons.org/licenses/by/3.0/deed.no>




Hapo zamani za kale, watu hawakujua chochote. Hawakujua kupanda mimea, hawakujua kushona nguo, wala hawakujua kuunda zana za chuma. Nyame, mungu aliyekuwa mbinguni, ndiye aliyekuwa mwenye hekima zote za dunia. Alihifadhi hekima hiyo kwenye chungu cha udongo.




Chungu kilivunjika vipandevipande pale chini. Hekima zikawa za bure kwa mtu yeyote kujichukulia. Na hivyo ndivyo watu walivyojifunza kulima, kushona nguo, kuunda zana za chuma, na mambo yote mengine ambayo watu wanajua kuyafanya.




Siku moja, Nyame aliamua kumpa Anansi chungu hicho cha hekima. Kila Anansi alipotazama ndani ya chungu cha udongo, alijifunza jambo jipya. Alifurahi sana!



Punde tu alipotika juu ya mti, aliwaza, "Natakiwa kuwa ndiye mwenye hekima zote, lakini hapa mwanangu ndiye mwenye akili kuliko mimi." Anansi alikasirishwa sana kiasi kwamba alikitupa kile chungu chini ya mti.



Anansi mlafi alinong'ona moyoni,
“Nitakificha chungu hiki juu ya mti mrefu
ili nikifaidi mwenyewe.” Akasokota uzi
mrefu na kuuzungusha kwenye chungu.
Kisha, akajifunga tumboni. Akaanza
kupanda kwenye mti. Lakini ilikuwa
vigumu kupanda kwenye mti huku chungu
kikimgonga magotini kila mara.



Wakati huo wote, mwanawe alikuwa
amesimama chini ya ule mti akimtazama
baba yake. Akamwambia, “Baba, si
ingekuwa rahisi kupanda endapo
ungekifungia chungu mgongoni?” Basi
Anansi akajaribu kukifungia chungu
kilichojaa hekima mgongoni mwake, na
kweli ikawa rahisi zaidi.